

## Pata habari zaidi

## Mafunzo bora ya Ualimu huzingatia mjumuisho na ulemavu

## Kila mtoto anahitaji mwalimu aliyefunzwa vizuri na anayezingatia mjumuisho

### Kampeni ya Ulimwengu kwa ajili ya Elimu

Tafuta habari zihusuzo harakati za kampeni hizi na pakua nyenzo za kampeni

[www.campaignforeducation.org](http://www.campaignforeducation.org)

### Mtandao wa Kuwezesha Elimu EENET

Pata makala kadhaa, ripoti, vipeperushi na vifaa ya kufunzia elimu mjumuisho na namna ya kuwasaidia walimu walio katika mjumuisho

[www.eenet.org.uk](http://www.eenet.org.uk)



© Marlies van der Kroft, Gushi Foundation / CDD

**Kila mtoto anahitaji kufundishwa na mwalimu anayetambua mahitaji ya mtoto huyo na kuelewa jinsi ya kumsaidia.**

### Wasiliana na IDDC

rue Washington 40

B-1050 Brussels

Belgium

Simu: +32 (0)2 644.43.23

Faksi: +32 (0)2 644.43.24

Barua pepe :info@iddcconsortium.net

Tovuti: [www.iddcconsortium.net](http://www.iddcconsortium.net)

**Kampeni ya Ulimwengu kwa ajili ya Elimu 2013** imeonesha haja ya kila mtoto kuwa na mwalimu aliyefunzwa vyema na anayewezeshwa vizuri. Kampeni hiyo imetaka sera na fedha kuelekezwa zaidi katika kuziba pengo kubwa lililopo la walimu bora waliosomea.

IDDC husaidia kufikia malengo ya kampeni hii na inataka kuhakikisha kwamba “ walimu waliosomea vizuri” na “mafunzo bora ya ualimu” yote hayo yanapewa nafasi muhimu katika mjumuisho na ulemavu.

Tunaamini kwamba:

- **Mwalimu aliyesomea vizuri ni yule mwenye uwezo wa kuwajumuisha wanafunzi wote pamoja na kuelewa namna ya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu.**
- **Mafunzo ya ualimu yatakuwa na ubora wa juu iwapo tu yatahusisha pia mafunzo yenye ufanisi kuhusu mjumuisho kwa ujumla na hususan mjumuisho wa wenye ulemavu.**

Walimu wote wanahitaji mafunzo ya ualimu ya kabla ya kuingia kazini na mafunzo kazini yahusuyo elimu mjumuisho. Pia wanahitaji mfumo wa usaidizi utakaowapa fursa ya kupatiwa msaada wa kitaalamu ili waweze kuhakikisha kwamba watoto wote, wakiwemo wale wenye ulemavu wanapata elimu bora pamoja na kushiriki kikamilifu katika kujifunza kuliko bora.


Katika kijarida hiki tunapendekeza mambo matano ya kuzingatia katika jitihada zako za kuingiza mjumuisho katika mafunzo ya ualimu na uajiri.

“Nilipotambua kuwa shule yangu inakuwa na kushirikisha watu wa aina mbali mbali, nilibaini kuwa mafunzo ya ualimu niliyoyapata hayakuwa ya kutosheleza. Niliamua kujifunza mjumuisho na kuwasaidia waalimu wengine walimu wengine”.



© SEEPD / EENET

“Najua kuwa ninaweza kufundisha vizuri zaidi kuliko wengi, lakini Chuo kinakosa vifaa na utaalamu wa kuwatathmini wanafunzi wenye ulemavu wa uoni kama mimi ”



© Peter Mwanyalo / EENET

“Sikuwahi kamwe kukutana na mtu mwenye ulemavu hadi pale nilipoanza kufundisha katika shule yenye mjumuisho”. Nilikuwa mwenye woga sana na sikuwa tayari”

**Kampeni ya ulimwengu kwa ajili ya elimu 2013 ilijikita katika mafunzo ya ualimu na uajiri.**

**Kipeperushi hiki kitakusaidia kuhusu suala muhimu la mjumuisho na ulemavu wakati ukifanya kampeni kwa ajili ya walimu zaidi na mafunzo bora ya ualimu**

# Mikakati mitano waweza zingatia ili kusaidia kufunza, kuajiri na kusaidia walimu kwa ajili ya mjumuisho

